# BEREAN CHRISTADELPHIANS NAMANJALALA ECCLESIA

SWAHILI HYMNS

Edit with WPS Office

## 1. AHADI ZILITOLEWA

Ahadi zilitolewa,
Kwanza kwa Ibrahimu,
Thibitisho kwa Isaka,
Na pia Yakobo.

Nchi, Uzao, Baraka,
Ahadi tatu muhimu,
Kwa baba zetu na sisi,
Tukilenga mbele.

Ibrahimu baba yetu,
Sisi uzao wake,
Tukiwa na Kristo,
Njia ya ubatizo.

Toka kaskazini,
Mashariki na kusini,
Kuja ufalmeni,
Ahadi kutimia.

Si mbinguni ni duniani,
Watakatifu kukaa,
Kufurahi milele,
Mbele ya masihi.

## 2. LIKO LANGO WAZI

Liko lango moja wazi,
Ni lango la Sayuni,
Na wote waingiao,
Watapata nafasi.

Lango ndiye Yesu Bwana,
Wote waingie kwake,
Lango! Lango! Lango! Lango!
La Sayuni li wazi.

Yesu ndiye lango hili,
Hata sasa li wazi,
Kwa wakubwa na wadogo,
Tajiri na maskini.

Hili ni lango la raha,
Ni lango la rehema,
Kila mtu apitaye,
Hana machozi tena.

Tukipita lango hili,
Tutatua mizigo,
Tuliyochukua kwanza,
Tutavikwa uzima.

## 3. YESU YUAJA KUTAWALA

Yesu yuaja tena,
Kutawala nchini,
Toka Yerusalemu,
Miisho ya dunia.

Leo dada yangu,
Nawe kaka yangu,
Tubu dhambi zako,
Bwana akusamehe.

Wale walio wake,
Watafurahi sana,
Maisha ya milele,
Yasiyo na mwisho.

Wale wasio wake,
Watahuzunika,
Pasipo namaisha,
Nchi ya giza tupu.

Mbinguni hatutaenda,
Ni mali ya Mungu,
Dunia tutakaa,
Watu wenye haki.

## 4. MANENO SABA YA MTINI

Maneno saba ya pale mtini,
Tuyaweke sana mioyoni mwetu,
Yatufunza kumtafuta mwokozi,
Aliyejifia ajiokoe.

Tumfuateni, tumfuateni,
Mwokozi mponya wetu,
Tumfuateni, tumfuateni,
Mwokozi mponya wetu.

Mwokozi wetu Yesu alisema,
Waache hawajui watendalo,
Mavazi wakayapigia kura,
Kama zamani walivyotabiri.

Ewe Yesu nikumbuke 'falmeni,
Yesu akajibu akamwambia,
Amini hivi leo tutakuwa,
Nawe mji ule wa paradise.

Tangu leo huyu ndiye  mamao,
Nawe mama huyu ndiye mwanao,
Maneno haya Yesu alisema,
Kwa uchungu wa kuwacha wapenzi.

Damu ilipotiririka sana,
Yesu akasema naona kiu,
Ndipo wakampa ile siki kali,
Akasema imemalizika.

Ee! Baba yangu,
Ipokee roho yangu,
Ee! Baba yangu,
Ipokee roho yangu.

Pale paitwapo fuvu la kichwa,
Yesu akalia kwa sauti kuu,
Eli! Eli! Lamasabakathan,
Mungu wangu mbona umeniacha.

Ilipokuwa yapata saa sita,
Pakawa na giza mpaka saa kenda,
Pazia la hekalu likapasuka,
Neno lake la mwisho lilikuwa.

## 5. MZABIBU WA KWELI

Mimi ndimi mzabibu wa kweli,
Na baba yangu ndiye mkulima.

Tawi ndani yangu lisilozaa,
Nitaliondoa na kulitupa.

Tawi lizaalo matunda mema.
Husafishwa ili kuzaa mengi.

## 6. BWANA U SEHEMU YANGU

Bwana u sehemu yangu,
Rafiki yangu wewe,
Katika safari yangu,
Tatembea na wewe.

Pamoja na wewe,
Pamoja na wewe,
Katika safari yangu,
Tatembea na wewe.

Mali hapa sikutaka,
Ili niheshimiwe,
Na yanikute mashaka,
Sawasawa na Yesu.

Pamoja na wewe,
Pamoja na wewe,
Na yanikute mashaka,
Sawasawa na Yesu.

Niongoze safarini,
Mbele nipumzike,
Mlangoni mwa Sayuni,
Niingie na wewe.

Pamoja na wewe,
Pamoja na wewe,
Mlangoni mwa Sayuni,
Niingie na wewe.

Edit with WPS Office

## 7. TWENDE KWA YESU

Twende kwa Yesu mimi nawe,
Atuonyeshe njia yake,
Imo chuoni na mwenyewe,
Hapa asema njoo.

Na furaha tutaiona,
Mioyo ikitakata sana,
Kwa ufalmeni kuonana,
Na milele kukaa.

Wana na waje atuambia,
Furahini mkisikia,
Ndiye mfalme wetu pia,
Na atuita njoo.

Wangoja nini leo yupo?
Sikiza sana asemapo,
Huruma yake ikuitapo,
Ewe kijana njoo.

## 8. KARIBU NA WEWE

Karibu na wewe,
Mungu wangu,
Karibu zaidi,
Bwana wangu,
Siku zote niwe.

Karibu na wewe,
Karibu zaidi,
Mungu wangu.

Mimi nasafiri,
Duniani,
Pa kupumzika,
Sipaoni,
Nila lapo niwe.

Yote unipayo,
Yanivuta,
Pa kukaribia,
Nitapata,
Na nielekezwe.

Na kwa nguvu zangu,
Nikusifu,
Mwamba, uwe maji,
Ya wokovu,
Mashakani niwe.

## 9. NDIYO DHAMANA

Ndiyo dhamana Yesu wangu,
Hunipa furaha za mbingu;
Mrithi wa wokovu wangu,
Nimezawa kwa Roho yake.

Habari njema raha ya yangu,
Yesu ndiye mwokozi wangu;
Habari njema raha yangu,
Yesu ndiye mwokozi wangu.

Kumsalimu moyo wangu,
Mara namwona raha yangu;
Aniletea malaika,
Wananilinda taokoka.

Hali na mali anitwaa!
Mara namwona anifaa;
Nami nangoja kwa subira,
Akiniita, nije mara.

## 10. NIPE RAHA MOYONI

Nipe raha moyoni nikusifu,
Nipe raha moyoni naomba,
Nipe raha moyoni nikusifu,
Nikusifu hata kucha.

Twimbe Hosana, twimbe Hosana,
Twimbe Hosana, mfalme mkuu!
Twimbe Hosana, twimbe Hosana,
Twimbe Hosana mfalme!

Nipe amani moyoni na upendo,
Nipe amani moyoni naomba,
Nipe amani moyoni na upendo,
Na upendo hata kucha.

Nipe upendo moyoni nitumike,
Nipe upendo moyoni naomba,
Nipe upendo moyoni nitumike,
Nitumike hata kucha.

## 11. MIKONONI MWA YESU

Mikononi mwa Yesu, kifuani mwake,
Mapenzi yanilinda, sina hofu kamwe;
Asha tuma wajumbe, kuleta habari,
Ya kutufurahisha, katika safari;

Mikononi mwa Yesu,
Kifuani mwake,
Mapenzi yanilinda,
Sina hofu kamwe.

Mikononi mwa Yesu, tashwishi sinayo;
Maonjo hayadhuru, madhambi hayamo.
Nikiwa na Mwokozi, siyoni majonzi;
Mashaka ni machache, machache machozi.

Yesu mwokozi wangu, akafa mtini;
Yesu mwamba wa kale, namtumaini.
Namngojea Bwana, mchunga rafiki;
Hata kupambauka, huko mashariki.

## 12. NIZIDI YESU KUMJUA

Nizidi Yesu kumjua,
Mapenzi yake kuyafanya,
Na nizidi kulijua,
Pendo la wokovu pia.

Zaidi ya Yesu,
Zaidi ya Yesu,
Nizidi kumjua sana,
Pendo la wokovu pia.

Nizidi nielimishwe,
Mapenzi yake niyatende,
Roho wa Mungu na uwe,
Mwalimu hata milele.

Nizidi katika neno,
Kushirikiana nalo,
Nisikie hilo neno,
Moyoni uwe msemo.

Nizidi kumwona Yesu,
Na utukufu wake kuu,
Akirudi kutoka juu,
Ufalme wake na uje.

## 13. MWAMBA MWENYE IMARA

Mwamba mwenye imara,
Kwako nitajificha,
Maji yale na damu,
Yaliyotoka humu,
Huziondoa dhambi,
Hunifanya mshindi.

Kwa kazi zote pia,
Sitimizi sheria,
Nijapofanya bidii,
Nikilia kwa kudhii,
Hayaishi makosa,
Ndiwe wa kuokoa.

Sina cha mkononi,
Naja mslabani,
Mimi tupu nivike,
Ni mnyonge nishike,
Mimi mchafu naja,
Nioshe sipotee.

Edit with WPS Office

## 14. NI TABIBU WA KARIBU

Ni tabibu wa karibu,
Tabibu wa ajabu,
Na rehema ya daima,
Ni dawa yake njema.

Imbeni malaika,
Sifa za Yesu Bwana,
Pekee limetukuka,
Jina lake Yesu.

Hatufai kuwa hai,
Wala kujitumai,
Ila Yesu kweli ndiye,
Atupumzishaye.

Dhambi pia na hatia,
Ametuchukulia,
Na twendeni na amani,
Hata msalabani.

Huliona tamu jina,
La Yesu Kristo Bwana,
Yuna sifa mwenye kufa,
Asishindwe na kifo.

## 15. NIMEHITAJI MWOKOZI

Nimehitaji mwokozi,
Awe nami daima,
Nataka mikono yake,
Kunizunguka sana,

Hofu rohoni sina,
Aniongoze tena,
Sitanung'unika tena,
Nimfuate daima.

Nimehitaji mwokozi,
Sina imani nyingi,
Atanifufusha moyo,
Wengine hawawezi.

Nimehitaji mwokozi,
Mwendoni mwa maisha,
Katika mateso mengi,
Tena katika vita.

Nimehitaji mwokozi,
Kiongozi njiani,
Kwa jicho aniongoze,
Nifikishe mwishoni.

## 16. WAMWENDEA YESU KWA KUSAFIWA

Wamwendea Yesu kwa kusafiwa
Na kuoshwa kwa damu ya kondoo?
Je! Neema yake atumwagiya?
Umeoshwa kwa damu ya kondoo?

Kuoshwa, kwa damu,
Itutakasayo ya kondoo?
Ziwe safi nguo nyeupe mno;
Umeoshwa kwa damu ya kondoo?

Wamwendea daima mkombozi,
Na kuoshwa kwa damu ya kondoo?
Yako kwa msulubiwa makazi;
Umeoshwa kwa damu ya kondoo?

Atakapokuja Bwana arusi,
Uwe safi kwa damu ya kondoo?
Yafaa eeh kumulaki Bwana Yesu;
Yafuliwe kwa damu ya kondoo?

## 17. NITWAE HIVI NILIVYO

Nitwae hivi nilivyo,
Umemwaga damu yako,
Nawe ulivyoniita,
Bwana Yesu naja, naja.

Hivi nilivyo si langu,
Kujiosha roho yangu,
Nisamehe dhambi zangu,
Bwana Yesu naja, naja.

Hivi nilivyo sioni,
Kamwe furaha moyoni,
Daima ni mashakani,
Bwana Yesu naja, naja.

Hivi nilivyo kipofu,
Maskini na mpungufu;
Wewe U mtimilifu,
Bwana Yesu naja, naja.

Nawe hivi utanitwaa,
Nisisubutu kukawa,
Na wewe hutanikataa,
Bwana Yesu naja, naja.

## 18. MUNGU AWE NANYI DAIMA

Mungu awe nanyi daima,
Hata twonane ya pili,
Awachunge kwa fadhili,
Mungu awe nanyi daima.

Mungu awe nanyi daima,
Ziwafunike mbawaze,
Awalishe awakuze,
Mungu awe nanyi daima.

Mungu awe nanyi daima,
Kila wakati wa zani,
Awalinde hifadhini,
Mungu awe nanyi daima.

Mungu awe nanyi daima,
Awabarikie sana,
Awapusilie kina,
Mungu awe nanyi daima.

## 19. CHAKUTUMAINI SINA

Cha kutumaini sina,
Ila damu yake Yesu,
Sina wema wa kutosha,
Dhambi zangu kuziosha.

Kwake Yesu nasimama,
Ndiye mwamba ni salama,
Ndiye mwamba ni salama.

Njia yangu iwe ndefu,
Yeye hunipa wokovu,
Mawimbi yakinipiga,
Nguvu zake ndizo nanga.

Damu yake na sadaka,
Nategemea daima,
Yote chini yakiisha,
Mwokozi atanitosha.

Nikiitwa hukumuni,
Rohoni nina amani,
Nikivikwa haki yake,
Sina hofu mbele zake.

## 20. SIOSHWI DHAMBI ZANGU

Sioshwi dhambi zangu,
Bila damu yake Yesu,
Hapendezewi Mungu,
Bila damu yake Yesu.

Hakuna kabisa,
Dawa ya makosa,
Ya kututakasa,
Ila damu yake Yesu.

La kunisafi sina,
Ila damu yake Yesu,
Wala udhuru tena,
Bila damu yake Yesu.

Sipati patanisho,
Bila damu yake Yesu,
Hukumu yanitisha,
Bila damu yake Yesu.

Yashinda ulimwengu,
Hiyo damu yake Yesu,
Yatupatanisha,
Hiyo damu yake Yesu.

JINA LA YESU SALAMA!

Edit with WPS Office

Jina la Yesu, Salama! Lisujudieni,
Ninyi mbinguni, hukumu,
Na enzi mpeni.

Enzi na apewe kwenu, watetea dini,
Mkuzeni Bwana wenu,
Na enzi mpeni.

Enyi mbegu ya rehema, nanyi msifuni,
Mmeponywa kwa neema,
Na enzi mpeni.

Wenye dhambi kumbukeni, ya msalabani,
Kwa furaha msifuni,
Na enzi mpeni.

Kila mtu duniani, msujudieni,
Kote-kote msifuni,
Na enzi mpeni.

## 21. JINA LAKE YESU TAMU

Jina lake Yesu tamu,
Tukilisikia,
Hutupoza tena hamu, hutuondolea.

Roho iliyoumia,
Kwalo hutibika,
Chakula njaani pia; raha tukichoka.

Jina hili ni msingi,
Ngao, ngome mwamba,
Kwa hili napata wingi, kwangu ni akiba.

Yesu mchunga rafiki,
Mwalimu kuhani,
Mwanzo, mwisho, njia, haki, uzima milele.

## 22. YESU ALINIITA

Yesu aliniita "Njoo!
Raha iko kwangu,
Kichwa chako ukilaze,
Kifuani mwangu,"
Nilikwenda kwake mara,
Sana nilichoka;
Nikapata kwake raha,
Na furaha tena.

Yesu aliniita "Njoo!
Kwangu kuna maji,
Maji ya uzima bure,
Unywe uwe hai,"
Nilikwenda kwake mara,
Na maji nikanywa;
Naishi kwake na kiu,
Kamwe sina tena.

Yesu aliniita "Njoo!
Dunia ina giza,
Ukinitazama nuru,
Takung'arizia,"
Nilikwenda kwake mara,
Yeye jua langu;
Ni kila wakati mwanga
Safarini mwangu.

## 23. USINIPITE MWOKOZI

Usinipite mwokozi!
Unisikie;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

Yesu, Yesu naomba, unisikie!
Unapozuru wengine,
Usinipite.

Kiti chako cha rehema,
Nakitazama;
Magoti napiga kwako,
Nisamehewe.

Sina wa kutegemea,
Ila wewe tu;
Uso wako uwe kwangu,
Nakuabudu.

## 24. MTETEENI YESU

Mteteeni Yesu,
Mlio askari;
Inueni beramu,
Mkae tayari;
Kwenda naye vitani
Sisi hatuchoki
Hata washindwe pia
Yeye amiliki.

Mteteeni Yesu,
Wenye ushujaa;
Nguvu zenu za mwili
Hazitatufaa;
Silaha ya injili
Vaeni daima;
Kesheni mkiomba;
Sirudini nyuma.

Mteteeni Yesu,
Vita ni vikali,
Wengi wamdharau,
Hawamkubali;
Ila atamiliki,
Tusitie shaka;
Kuwa naye vitani,
Twashinda hakika.

## 25. YESU KWETU NI RAFIKI

Yesu kwetu ni rafiki,
Twambiwa aja pia;
Tukiomba kwa Babaye,
Maombi asikia.
Lakini twajikosesha,
Twajitweka vibaya;
Kwamba tulimwomba Mungu,
Dua angesikia.

Una dhiki na maonjo?
Una mashaka pia?
Haifai kufa moyo,
Dua atasikia.
Hakuna mwingine mwema,
Wa kutuhurumia;
Atujua tu dhaifu;
Maombi asikia.

Je! Hunayo hata nguvu,
Huwezi kwendelea
Ujapodharauliwa
Ujaporushwa pia.
Watu wangekudharau,
Wapendao dunia,
Hukwambata mikononi,
Dua atasikia.

## 26. YOTE NAMTOLEA YESU

Yote namtolea Yesu,
Nampa moyo wote,
Nitampenda siku zote,
Namwandama kila saa.

Yote kwa Yesu,
Yote kwa Yesu,
Yote kwako eh! Mwokozi
Namwandama tu.

Yote namtolea Yesu,
Nainamia kwake,
Nimeacha na anasa,
Kwako Yesu nakupenda.

Yote nakutolea Yesu,
Nipe nguvu eh! Bwana,
Nifanye niwe wako,
Unilinde daima.

Yote namtolea Yesu,
Nami naona sasa,
Furaha ya ukombozi,
Nasifu jina lake.

## 27. UNIAMBE YA YESU

Edit with WPS Office

Uniambie ya Yesu,
Nayafahamu sana,
Maneno yake matamu,
Yenye thamani sana;
Yesu alipozaliwa,
Waliimba mbinguni,
Mungu atuzwe juu,
Amani duniani,

Uniambiye ya Yesu,
Niyafahamu sana,
Maneno yake matamu,
Yenye thamani sana.

Njaa aliona nyikani,
Siku arobaini,
Alijaribiwa sana,
Akayashinda yote,
Kazi kufanya kwa nguvu,
Mateso kawa nayo,
Watu walimdharau.

Ndipo alisulubiwa,
Akaumizwa sana,
Akafa na akazikwa,
Tena akafufuka,
Upendo huu wa ajabu,
Faida nina kwangu,
Naushukuru upendo,
Ulioniokoa.

## 28. HAPANA RAFIKI KAMA YESU

Hapana rafiki kama Yesu
Yu pekee! Yu pekee!
Hapana mpozi kama Yesu
Yu pekee! Yu pekee!

Yesu ajua shida zetu,
Aweza kutuongoza,
Hapana rafiki kama Yesu,
Yu pekee! Yu pekee!

Nani mwingine amushinda Yesu?
Yu pekee! Yu pekee!
Tena ni nani mnyenyekevu?
Yu pekee! Yu pekee!

Nani pamoja nasi daima?
Yu pekee! Yu pekee!
Kwa usiku aleta salama;
Yu pekee! Yu pekee!

## 29. KAA NAMI NI USIKU TENA

Kaa nami ni usiku tena,
Usiniache gizani, Bwana,
Msaada wako haukomi,
Nili pekee yangu, kaa nami.

Siku zetu hazikawii kwisha,
Sioni la kunifurahisha,
Hakuna ambacho hakikomi,
Usiye na mwisho kaa nami.

Nina haja nawe kila saa,
Sina mwingine wa kunifaa;
Mimi nitaongozwa nani?
Ila wewe Bwana, kaa nami.

Siachi neno, uwapo karibu,
Nipata lolote si taabu,
Kifo na kaburi haviumi,
Nitashinda kwako kaa nami.

## 30. MUNGU MTUKUFU

Mungu mtukufu aliye Baba,
Akamtoa Yesu mpendwa mwana,
Akawa dhabihu kwa dhambi zote,
Kufungua njia kwa watu wote.

Msifuni msifuni,
Nchi imsikie,
Msifuni msifuni.
Bwana mshangilie,
Njooni kwake Bwana,
Kwa Yesu mwana,
Mpeni heshima aliye Bwana.

Ukombozi wetu tendo la Mungu,
Na ukamilifu kwa kila mtu,
Mwenye ukosefu akimwamini,
Atasamehewa na Yesu kweli.

Ametufundisha mambo ya mbingu,
Tukafurahishwa mwana wa Mungu,
Ametuinua karibu naye,
Atatungoza hata milele.

## 31. NJOONI KWA FURAHA

Njooni na furaha,
Enyi wa Imani,
Njooni Bethelehemu upesi,
Amezaliwa jumbe wa mbinguni.

Njooni tumuabudu,
Njooni tumuabudu,
Njooni tumuabudu,
Mwokozi.

Ona wachungaji,
Penye hori yake,
Kundi kuacha pole pole nasi tuende,
Nyayo tuzifuate.

Jeshi la mbinguni,
Imbeni kwa nguvu,
Mbingu zote na zijae sifa!
Sifuni Mungu aliye mbinguni.

## 32. WACHUNGA WALIPOLINDA

Wachunga walipolinda,
Kuacha nyama zao,
Malaika mtukufu,
Alishuka kwao.

Wakaja sana wachunga,
Akawatuliza,
Nawaletea habari,
Ya kuwapendeza.

Mji ule wa Daudi,
Leo amezaliwa,
Mwokozi ni Kristo Bwana,
Ilivyoandikwa.

Huyo mwana wa mbinguni,
Ataonekana,
Amelazwa kihorini,
Malazi hapana.

Walipokwisha yanena,
Malaika hao,
Waliimba wimbo huu,
Usio na mwisho.

Enzi ni yake Mungu juu,
Na nchi salama,
Kwa watu radhi kuu,
Sasa na daima.

## 33. NI SIKU KUU

Ni siku kuu siku ile,
Ya kumkiri mwokozi,
Moyo umejaa tele,
Kunyamaza hauwezi.

Siku kuu! Siku kuu!
Ya kuosha dhambi zangu kuu,
Kukesha na kuomba tu,
Ananiongoza miguu,
Siku kuu! Siku kuu!
Ya kuosha dhambi zangu kuu.

Tumekwisha kupatana,
Mimi wake yeye wangu,
Na sasa nitamwandama,
Nikiri neno la Mungu.

Moyo tulia kwa Bwana,

Edit with WPS Office

Kiini cha raha yangu,
Huna njia mbili tena,
Yesu ndiye njia yako.

## 34. MUSALABANI PA MWOKOZI

Msalabani pa mwokozi,
Hapo niliomba upozi,
Akaniokoa mpenzi,
Mwana wa Mungu.

Mwana wa Mungu,
Mwokozi wangu,
Akaniokoa Mpenzi,
Mwana wa Mungu.

Chini ya mti msumbufu,
Niliombewa wokovu,
Alinikomboa na damu,
Mwana wa Mungu.

Mwana wa Mungu,
Mwokozi wangu,
Alinikomboa na damu,
Mwana wa Mungu.

Aliniokoa dhambini,
Ikawa kunikaa ndani,
Aliponifia mtini,
Mwana wa Mungu.

Mwana wa Mungu,
Mwokozi wangu,
Aliponifia mtini,
Mwana wa Mungu.

## 35. MLE KABURINI

Mle kaburini, Yesu mwokozi,
Alilazwa chini, Bwana wangu .

Alifufuka Bwana,
Mauti alishinda sana,
Akatoka gizani mle chini,
Sasa amekaa juu mbinguni,
Yu hai, yu hai.
Bwana Yesu yu hai.

Alingoja humo, Yesu mwokozi,
Mchana ujao, Bwana wangu .

Walinda kaburi, Yesu mwokozi,
Walilinda bure, Bwana wangu.

Kifo kimeshindwa, Yesu mwokozi,
Pingu imevunjwa, Bwana wangu.

## 36. HUYO NDIYE!

Huyo ndiye! Anashuka,
Yeye alitufia!
Wengi waliookoka,
Watamfurahia,
Haleluya! Haleluya!
Yesu aturudia.

Sote tutamtazama,
Amekaa kitini,
Nao waliomchoma,
Kumkaza mtini,
Na kilio, na kilio,
Wamwone enzini!

Watasujudia wote,
Mbele ya kiti chako!
Zako, Bwana, nguvu zote,
Twae miliki yako!
Njoo Bwana, njoo Bwana,
Sisi tu watu wako.

## 37. FURAHA KWA ULIMWENGU

Furaha kwa ulimwengu,
Bwana atakuja,
Nyote mkaribisheni,
Mioyo yenu na mpeni,
Wote wamshangilie,
Wote wamshangilie,
Wote, na wote wamshangilie.

Furaha kwake duniani,
Mwokozi ni mfalme,
Bonde, mulima na mwamba,
Maji, mitoni na shamba,
Rudisheni sauti,
Rudisheni sauti,
Rudisheni, na rudisheni sauti.

Dhambi zisiongezeke,
Wala uhalifu,
Yuaja kutubariki,
Atuletea ushindi,
Kuharibu dhambi,
Kuharibu dhambi
Kuharibu, na kuharibu dhambi.

Atawala na neema,
Kwao mataifa,
Utukufu na waone,
Haki yake itendeke,
Kwa upendo wake,
Kwa upendo wake,
Kwa upendo, na kwa upendo wake.

## 38. BABA YETU ALIYE MBINGUNI

Baba yetu aliye mbinguni,
Amenifurahisha yakini,
Kuniambia mwake chuoni,
Ya kuwa nami Yesu pendoni.

Anipenda, Mwokozi Yesu,
Anipenda, anipenda,
Anipenda, Mwokozi Yesu,
Anipenda mimi.

Nimuachapo kutanga mbali,
Yeye yu vivyo hupenda kweli,
Hunirejeza kwake moyoni;
Kweli yu nami Yesu pendoni.

Haya kujua yanipa raha,
Kumuamini kuna furaha,
Huyapunguza mara mashaka,
Kwona yu nami Yesu pendoni.

Anipenda! Nami nampenda,
Kwa wokovu alionitenda,
Akanifia pale mtini,
Kwa kuwa nami Yesu pendoni.

## 39. NIMEAHIDI YESU

Nimeahidi Yesu,
Kukutumikia,
Wewe u Bwana wangu,
U rafiki pia,
Sitaogopa vita,
Wewe ndiwe mweza,
Sitaicha njia,
Ukiniongoza.

Imbeni haleluya!
Haleluya! Imbeni,
Shangwe kwa Bwana Yesu,
Ndiye mweza wetu.

Dunia i karibu,
Bwana siniache,
Na mengi majaribu,
Yako pande zote,
Siku zote adui,
Ni ndani na nje,
Bwana Yesu nivute,
Karibu na wewe.

Nikusikie wewe,
Nena nami Bwana,
Kelele za dunia,
Ndizo nyingi sana,
Nena kunihimiza,
Au kunionya,
Nena nikusikie,
Mwenye kuniponya.

Umewapa ahadi,

Edit with WPS Office

Wakufuatao,
Wawe ulipo wewe,
Nawe uwe nao,
Nami nimeahidi,
Kukutumikia,
Nipe neema Bwana,
Ya kukwandamia.

## 40. TWENDENI ASKARI

Twendeni askari,
Watu wa Mungu,
Yesu yuko mbele,
Tumwandame tu,
Ametangulia,
Bwana vitani,
Twende mbele kwani,
Ndiye amini.

Twendeni askari,
Watu wa Mungu.
Yesu yuko mbele, tumwandame tu.

Kweli kundi dogo,
Watu wa Mungu,
La mababa wetu,
Ni letu fungu,
Hatutengwi nao,
Moja Imani,
Tumaini moja,
Na moja dini.

Haya mbele watu,
Nasi njiani,
Inueni mioyo,
Nanyi sifuni,
Heshima na sifa,
Ni ya mfalme,
Juu hata chini,
Sana zivume.

## 41. MSINGI WA KANISA

Msingi wa kanisa,
Ndiye Yesu Bwana,
Kiumbe kipya chake,
Aipenda sana,
Kutaka itafuta,
Alishuka hapa,
Naye kwa haja yake,
Akafa Bwana.

Ina kila kabila,
Kisha ndiyo moja,
Wakovu wake una,
Mwokozi mmoja,
Uzazi ni umoja,
Ni moja Imani,
Chakula ni kimoja,
Moja tumaini.

Watu hustaajabu,
Kwa mashaka yote,
Yaipatayo nje,
Hata ndani mote,
Ila watakatifu,
Huomba, wakikesha
Usiku ni kilio,
Asubuhi raha.

Mashaka na taabu,
Hata vita vyake,
Vyangoja matimizo,
Ya amani yake,
Ndipo kwa macho yetu,
Tuone utukufu,
Kanisa ya kushinda,
Pamoja na Bwana.

## 42. NI UJUMBE WA BWANA

Ni ujumbe wa Bwana, haleluya!
Wa maisha ya daima,
Amenena mwenyewe, haleluya!
Utaishi ukimtazama.

Tazama! Ishi sasa!
Kumtazama Yesu,
Amenena mwenyewe, haleluya!
Utaishi ukimtazama.

Ni ujumbe wa pendo, haleluya!
Rafiki eh! Ni wako,
Unatoka juu huko, haleluya!
Mwenye ujumbe ni Yesu.

Uzima watolewa, haleluya!
Uzima wa daima,
Ukimtazama haleluya!
Pekee yake anaponya.

## 43. YESU ATAKA KIANGA

Yesu ataka kianga,
Kung'ara daima,
Kwa Yesu niwe kianga,
Popote daima.

Kianga, kianga,
Kwa Yesu niwe kianga,
Kianga, kianga,
Niwe kianga kwake.

Niwe mpenzi wa Yesu,
Niwapende wote,
Kuwaonyesha wengine,
Pendo siku zote.

Bwana Yesu, nimuulize,
Anisaidie,
Moyo wangu utakaswe,
Naye siku zote.

Niwe kianga kwa Yesu,
Kuwa mwaminifu,
Nitumike naye Yesu,
Kisha nitamsifu.

## 44. YESU NIWE KARIBU

Yesu niwe karibu,
Msalaba wako,
Uniponye kwa damu,
Yako ya kalvari.

Kalvari, kalvari,
Utukuzwe kwangu,
Hata roho ipate,
Raha huko kwako.

Kwa pendo na rehema,
Ulinitafuta,
Mwanga wa wokovu,
Ulizunguka.

Bwana niwe kila saa,
Mikononi mwako,
Nikumbushe daima,
Maumivu yako.

## 45. NADUMU KWA AHADI

Nadumu kwa ahadi zake mfalme,
Yesu asifiwe kwa siku zote,
Nitamwimbia sana, atukuzwe,
Kudumu kwa ahadi zake.

Dumu, dumu,
Dumu kwa ahadi za Mungu mwokozi wangu
,
Dumu, dumu,
Nadumu kwa ahadi za Mungu.

Nadumu kwa ahadi sina shaka,
Ahadi zisizokosa kabisa,
Kwa neno la Mungu nitashindaa,
Kudumu kwa ahadi zake.

Nadumu kwa ahadi nafahaamu,
Nina utakaso mkamilifu,
Kudumu kwa uhuru wake Yesu,
Kudumu kwa ahadi zake.

Kudumu kwa ahadi zake Kristo,
Kwa milele nimefungwa na pendo,
Nitashinda kwa upanga wa Roho,
Kudumu kwa ahadi zake.

Edit with WPS Office

## 46. UJIRUSHWA – RUSHWA

Ujirushwa – rushwa na dunia hii,
Utakapokufa moyo kwa kudhii,
Zilizo Baraka zihesabu tu,
Nawe utaona ni ajabu kuu.

Zilizo Baraka zihesabu tu,
Mungu aliyofanya ndiyo makuu,
Zilizo Baraka zihesabu tu,
Nawe utaona ni ajabu tu.

Haya basi ndugu twende mbele tu,
Na tusife moyo Mungu ni mkuu,
Hesabu baraka nawe ungojee,
Hata mwisho atakuwa na wewe.

## 47. ANIPENDA NI KWELI

Anipenda ni kweli,
Mungu anena hili,
Sisi wake watoto,
Kutulinda si zote.

Yesu anipenda,
Yesu anipenda,
Kweli anipenda,
Mungu amesema.

Kwa kupenda akafa,
Niokoke na kufa,
Atazisafi taka,
Sana ataniweka.

Anipenda kabisa,
Niuguapo sasa,
Anitunza mbinguni,
Niliyelala chini.

Kunipenda haachi,
Tu sote hapa chini,
Baada ya mashaka,
Nitaishi milele.

## 48. WATUMWA WA BWANA

Watumwa wa Bwana,
Na wakae vyema,
Walitii neno sana,
Wakeshe daima.

Taa tengezeni,
Kwa mafuta tele,
Vyuno vyenu jifungeni,
Mwenende na mbele.

Anena kesheni,
Mwombapo ni papo,
Mkono utazameni,
Mje upungapo.

Una heri wewe,
Hivi ukikaa,
Uso wake utazame,
Taji utavaa.

Atandika meza,
Mfame kwa wake,
Tena atawatukuza,
Wateule wake.

## 49. DUNIA NZIMA INASIKITISHA

Dunia nzima inasikitisha,
Na huu ulimwengu, unayo mashaka,
Nitafanyaje, mimi eeh kiumbe,
Bwana akija kunihukumu.

Ninayoyafanya, ninayoyaona,
Ninayofikiri, Bwana ni ubatili,
Roho yangu Yesu, Bwana nakuomba,
Uitunze vyema, milele na milele.

Eeh! Mungu wangu, mimi nakuomba,
Unipokee, mimi mwenye dhambi,
Ya dunia hii, mimi yanishinda,
Eeh! Mungu wangu, unipokee.

Naigopa, siku yake Bwana,
Akija kuhukumu, ulimwengu,
Watendao dhambi, hawatamuona,
Walia na kushaga, meno yao.

## 50. MUSA ALIYENDA MLIMANI MWA SINAI

Musa liyenda mlimani mwa Sanai,
Aliyenda kusema na Mungu,
Alipokawia kurudi toka huko,
Waisaraeli walishangaa!
Wakamkemea Haruni wakisema,
Musa wako ametudanganya,
Alitutoa huko nchi ya Misri,
Sasa mwenyewe ameshafariki.

Waisraeli ni walishangaa,
Na wala hawakukumbuka,
Ishara zote Bwana Mungu alifanya.

Ututengezee sanamu ya dhahabu,
Hiyo itakuwa Mungu wetu,
Sisi hatumuoni huyu Mungu wenu,
Twawezaje kumtumikia?
Haruni akafanya alivyoamuriwa,
Akawatengezea sanamu,
Na walipokuwa wakifanya sherehe,
Musa akatoka mlimani.

Mungu na Musa waligadhabika sana,

Musa akavunja sanamu hiyo,
Akawalazimisha kunywa maji yaliyo,
Changanywa na unga wa sanamu.
Usiwe na Mungu mwingine ila mimi,
Ewe mwanadamu sikiliza,
Hiyo ni sauti ya Mungu mwenyezi,
Aliyetuumba wewe nami.

## 51. JUKUMU LETU SISI KINA MAMA

Jukumu letu sisi kina mama,
Ni kuwahubiria,
Wanadamu watoke dhambini,
Nuru ya Bwana iwangazie.

Njoo Bwana ni nuru,
Nuru ya ulimwengu,
Tokeni gizani,
Nuru ya Bwna iwangazie.

Matendo yako ewe Mwanadamu,
Ni mema yaonekana,
Lakini mbele ya Mungu si mema,
Utasema nilijikwaa Bwana.

Dunia imejawa na maovu,
Wanandamu wateseka,
Wamekua mateka ya maovu,
Kweli dunia yaangamia.

## 52. SISI NI BARUA YAKE MUNGU

Sisi ni barua yake Mungu,
Twasomwa na watu wote duniani,
Sisi ni watu wa Yesu,
Twaonekana kokote,
Kwamba sisi ni barua ya Bwana.

Tuwe kielelezo sisi,
Uwe nuru ya kweli wewe,
Uwe tume njema,
Tena uwe barua,
Usomwe na watu wote duniani, wewe.

Sisi ndiyo mashahidi wake,
Bwana Yesu asema sikiliza,
Matendo yetu mazuri,
Yasomwe na watu wote,
Ili Mungu atukuzwe kokote.

Tazama siku ya Bwana yaja,
Tukaposomwa sote pamooja,
Ukiwa barua njuri,
Utasomwa vyema,
Barua mbaya itachanwa na kutupwa.

## 53. MACHO YAKE MUNGU YANAONA KOTE

Edit with WPS Office

Macho yake Mungu yanaona kote,
Juu ya mlima, hata na angani,
Nawe mwanadamu unafikiria,
Mungu hakuoni utendapo dhambi.

Yote ufanyayo, hata usemayo,
Hata yale yote unanaficha watu,
Yataonekana juu ya mlima,
Rekebisha mwendo hukumu yaja.

Neno lake Mungu lasema wazi,
Tukifanya dhambi tutakuwa wafu,
Bali tukifanya yampendezayo,
Tutazipokea ahadi za uzima.

Mungu aliupenda ulimwengu sana,
Kamtoa mwana wake wa pekee,
Ili tumwamini tusipotee,
Bali tuurithi ufalme wake.

## 54. KAZI YAKE BWANA YESU HUMU DUNIANI

Kazi yake Bwana Yesu humu duniani,
Ilipangwa kuanzia mwanzo,
Na Yohana alitangulia,
Mbele yake, kuhubiri injili ya toba,
Alipaza sauti yake kuu akisema,
Msamaha umekuja kwenu.

Tengeneza njia yake Bwana,
Yanyosheni, nyosheeni mapito yake,
Tubu dhambi ubatizwe kwa maji,
Ungoje, ubatizo wa Roho na moto.

Na Yohana, akasema yupo nyuma yangu,
Yuaja aliye na nguvu,
Na kiatu cha mguu wake,
Sitaweza kukiguza kwa mkono wangu,
Huyu Yesu anao uwezo,
Tutapata ubatizo wa Roho na moto.

Je wanena, nini kuhusu watu wa Mungu?
Wainue mbele zake Mungu,
Waheshimu umuone Mungu,
Akitenda kazi ndani mwao,
Kama vile Yohana alivyonena vyema,
Kumhusu Yesu mwana wake.

## 55. MATAIFA YATAKUSANYWA

Mataifa yatakusanywa,
Mbele yake Yesu mwokozi.

Itika Bwana wangu,
Itika Bwana wangu,
Taja Bwana,
Tamka Bwana wangu.

Aliyahidi kuwalinda ,
Watakatifu mpaka siku ile.

Atahukumu kila mmoja,
Kulingana na matendo yake.

Nikilio kwa wale wote,
Wa mkono wake wa kushoto.

## 56. ILIKUWA SIKU MOJA JIONI

Ilikuwa siku moja jioni Luti alipata wageni,
Na wageni walimpasha habiri,
Kwamba Sodoma itachomwa na moto.

Sodoma itachomwa, pamoja na Gomora,
Hiyo ni siri kubwa, ya mbinguni,
Moto utashuka, utatatoka wapi Luti,
Wa kuangamiza Sodoma na majengo yake,
Luti umeelewa.

Naye mkewe Luti,
Alivunja hilo agizo,
Walilopewa na Mungu.

## 57. BWANA YESU ALIENDA MLIMANI

Bwana Yesu alienda,
mlimani mwa msituni,
Aliporudi hekaluni,
watu wote wakaja kwake.

Mafarisayo na waandishi,
Walimuleta mwanamke mbele ya Bwana,
Ahukumiwe na Bwana Yesu,
Walikuwa wakimjaribu.

Mara wote wakangojea,
Jibu la Bwana kwa mwanamke,
Akainimisha kichwa chake,
Na kuyafikiri majaribu.

Mara Yesu akainua,
Kichwa chake na kuwajibu,
Yule ambaye hajakosa,
Na ampige kwa jiwe la kwanza.

## 58. ANAKUJA KUOKOA

Anakuja kuokoa sasa songa karibu,
Anakuja utasikia tarumbeta ikilia.

Tarumbeta italia mwakozi anarudi,
Wacheni dhambi,
Wewe wategemea bado wafanya dhambi,
Wewe utakuwa wapi siku hiyo?

Anakuja kuokoa sasa songa karibu,
Anakuja kukupata kama wewe huna nguo.

Sisi tumepata sauti ikisema,
Turudi haraka mwokozi anarudi.

## 59. BWANA YESU ALIPOKUWA

Bwana Yesu alipokuwa,
Hapaduniani nasi,
Alisema jambo moja,Tufanye jambo moja,
Tukimkumbuka yeye.

Yesu akachukuwa mkate,
Akashukuru akawapa wanafunzi wake,
Akasema chukueni mleni,
Mwili wangu, ni mwili wangu.
Tena akachukuwa divai,
Akashukuru akawapa wanafunzi wake,
Akasema chukueni mnyweni,
Damu yangu, ni damu yangu.

Damu hiyo ya Bwana,
Aliyoimwaga msalabani,
Ilikuwa ya kuweka,
Uhusiano wetu na Mungu.

Tukitenda dhambi tena,
Twamsulubisha tena,
Mbona mwaga damu tena,
Kwa maovu yetu.

Ukibatizwa kwa jina lake,
Wewe ni mtoto wake,
Tena ndugu wa Yesu,
Tufanye alivyotuagiza.

## 60. YESU ALIENDA GETHSEMANI

Yesu aliyenda Gethsemani,
Na walimu na Petro,
Na wale watoto wa Zebedayo.

Hapo akaanza kuzungumza,
Akawambia mkae macho,
Moyo unapenda lakini mwili,
Lakini mwili umekwisha nguvu.

Yesu alikuwa akizungumza,
Yuda akaja na jeshi lake,
Pamoja na jeshi la wateza nyuma.

Yuda akaja na jeshi lake,
Akawambia mmukamate,

Edit with WPS Office

Ndiye huyu Bwana mmkamate.

Wale majeshi wakamshika,
Naye Petro akatoa panga,
Naye Bwana Yesu akamwambia,
We petro usitoe panga.

## 61. NITAKUTUKUZA EEH MUNGU

Nitakutukuza eeh1 Bwana,
Mungu wa Ibrahimu,
Nitakuimbia Bwana wetu,
Mungu wa Yakobo.

Shangwee! Shangwee!
Shangwee! Shangilieni,
Bwana Mungu wee! Mungu wa neema,
Mungu wa upendo, Mungu wa uzima,
Mungu wa uwezo, Mungu wa neema.

Alimbariki Daudi,
Pamoja na Isaka,
Tukifanya mapenzi yake,
Tutabarikiwa tele.

Tuangalie Abramu,
Pamoja na Sarai,
Mwana mvulana wakapewa,
Wakiwa wazee sana.

Shida zetu za dunia,
Yeye azijua,
Bora kwake  kwa maombi,
Yote atatuwezesha.

## 62. DUNIA NI BAHARI

Dunia ni bahari,
Dhambi nazo mawimbi,
Chunga sana bahari,
Usizame majine.

Ewe tembea,
Mwana wangu tembea,
Ewe tembea,
U majini tembea.

Bwana nipe uwezo,
Kama Petero Simioni,
Niwe juu ya maji,
Nisizame majini.

Fanya kazi ya Bwana,
Ungali bado kijana,
Umeitwa na Bwana,
Uhubiri neno lake.

## 63. EWE NDUGU

Ewe ndugu, mmh! Mmh!
Kumbuka ya kwamba,
Bwana anakupa vitu vyake bure,
Anakulinda usipate taabu,
Na wewe ndugu ni wakati wako,
Ujiulize.

Kweli Yesu, ni mkombozi,
Ana hata, ana huruma nyingi,
Badala yeye, huchukizwa,
Na dhambi zetu, tunazofanya,
Kweli atwita twende kwake.

Ewe ndugu, mmh! Mmh!
Utaionaje?
Ukiulizwa kumtoa mwana,
Wako mpendwa uliye naye,
Afe kwa ajili ya ukombozi,
Utajibuje?

Ewe ndugu, mmh! Mmh!
Tupige magoti,
Tumulilie aliyetupenda,
Akateswa na kupigwa sana,
Na mwanadamu kule kalivari,
Ili tukombolewe.

## 64. MIMI NDIYE WA KWANZA

Mimi ndiye wa kwanza tena na wa mwisho,
Usiwe naye Mungu mwingine kabisa,
Ndivyo anavyosema Bwana wa majeshi,
Mungu mtakatifu mwenye nguvu zote.

Mimi nitampa yule mali ya uzima ule,
Yule atakayeshinda ya dunia haya yote,
Atakuwa ndani yangu hata mimi ndani yake,
Kwenye utukufu ule tutaimba haleluya.

Mimi nilikuumba unitumikie,
Katika siku zote hapa duniani,
Mbona sasa wawacha njia ya uzima,
Waifwata dunia itakupoteza.

Wacha udanganyifu twenda kwake sasa,
Yeye ni wa rehema tena wa upole,
Machozi yetu yote yeye atafuta,
Tutakapomwendea na kutubu kweli.

## 65. MUNGU FUNGUA MLANGO

Mungu fungua, mlango nipate kuingia,
Mlango umefungwa, nenda zako sikujui!

Mzee wa kanisa, mmh!
Mimi ni mhubiri, aah!
Mimi ni mchungaji, nenda zako sikujui!

Wengine watasema, tulikuwa wanakwaya,
Na Mungu atasema, nenda zako sikujui!
Sadaka nilitoa, Biblia nilisoma,
Na Mungu atasema, nenda zako sikujui!
Hekalu nilijenga, hata mawe niliweka,
Na Mungu atasema, nenda zako sikujui!

## 66. VIPOFU WAWILI

Vipofu wawili waliketi njiani,
Waliposikia Yesu anapita,
Walipaza sauti tena wakisema,
Uturehemu Bwana mwana wa Daudi.

Walipaza sauti,
Walipaza sauti,
Walipaza sauti tena wakisema,
Uturehemu Bwana mwana wa Daudi.

Yesu aliposikia wakimlilia,
Aliwahurumia wote wawili,
Walipaza sauti tena wakisema,
Uturehemu Bwana mwana wa Daudi.

## 67. WACHUNGA WALIPOLINDA

Wachunga walipolinda,
Kuacha nyama zao.

Kweli waliona nuru,
Nuru mkubwa sana,
Kweli wakaja sana,
Malaika akaonekana.
Mmmmmh!
Mmmmmh!
Mmmmmh!
Malaika akaonekana.

Tuliona nyota zao,
Katika mashariki.

Mamajusi walipofika,
Katika Yerusalemu.

## 68. JITAHIDI SANA

Jitahidi sana uingie,
Kwenye mlango mwembamba,
Mwisho wa safari ni uzima,
Pamoja naye mwokozi.

Kweli njia ni nyembamba,
Ieandayo Sayuni uzimani,
Jitahidi sana uingie,
Kwenye mlango mwembamba.

Jitahidi fanya bidii ndugu,
Upitie njia hiyo,
Hata ikiwa ni nyembamba
Ndiyo njia ya uzima.

Tazama Yesu msalabani,
Mwanzilishi wa njia,

Edit with WPS Office

Damu yake ilimwagika,
Nawe safari salama.

## 69. SIKU ILE YA KWANZA

Siku ile ya kwanza Yesu kasulubiwa,
Alikuwa ameketi na wafuasi wake,
Kati yao hawakuweza kumtambua,
Atakayemsaliti.

Wafuasi walianza na kutazamana,
Ni nani atakaye kumsaliti Yesu,
Kati yao hawakuweza kumtambua,
Atakayemsaliti.

Yesu aliposulubiwa wakati ule,
Aliyetenda hayo ni mfuasi wake,
Wakristo wote Yerusalemu walishangaa,
Yuda Iska amefanya nini?

Kumbe Yuda wa siku zile bado yupo,
Kila tutembeapo anatufuata nyuma,
Atudanganya eti yeye ni mmoja wetu,
Kumbe yeye ni msaliti.

Yule aliyefikiriwa asiye kosa,
Kila mara yuaketi karibu na Yesu,
Kumbe moyoni mwake anayo hila mbaya,
Kumwangusha asiye na kosa.

## 70. YESU ALIPOKAMATWA

Yesu alipokamatwa, kwenda kusulibiwa,
Wanafunzi wake wote, walishikwa na hofu,
Walitimua mbio, wamesahau ya kwamba,
Baada ya hayo yote, watapata ushindi.

Jiwe kubwa, likaviringishwa,
Kwenye lango, ulinzi mkubwa,
La ajabu ni kwamba, Yesu alifufuka,
Mauti yakashindwa, kumzuia Bwana.

Yesu aliwambia, msiwe nayo hofu,
Mnamuamini Mungu, niamini na mimi,
Nyumbani mwa baba yangu, mna makao mengi
Kama ingekuwa sivyo, nisingeliwambia.

Mimi naenda kwa Baba, kuandaa makao,
Na hivyo sitawawacha, mukiwa yatima,
Nitatuma mshauri, mshauri wa ajabu,
Atawapa nguvu mpya, kutangaza injili.

## 71. ESIE MENYANGA ATINYU

Esie menyanga atinyu,
Engo yanje yararira,
Shiyombokhwa khumuyetse,
Yombokhwa khulwanda.

Yombokhwa khulwanda,
Olwanda lutinyu
Shiritsanya olutseka,
Yombokhwa khulwanda.

Olwe shibi shikwitsanga,
Shinga imbutsa ingari,
Ndamanya ovwa ndasubira,
Yombokhwa khulwanda.

Olwe tsinyumba tsindi,
Tsikwitsanga ni chirwa,
Enyumba yanje yatinya,
Yombokhwa khulwanda.

Enyanga yange niyula,
Ndi neyinyumba Sayuni,
Ndabikhayo mwoyo kwanje,
Yombokhwa khulwanda.

## 72. KATIKA MJI WA TARISO

Katika mji wa Tariso,
Mji wa kililio,
Palikuwa na kijana mmoja,
Jina lake sauli.

Sauli! Sauli!
Kijana wa Tariso,
Alikuwa mtesi,
Kaomba barua,
Kuwatesa wakristo.

Sauli alitesa watu,
Wanaume na wake,
Kawapeleka gerezani,
Kule Yerusalemu.

Alipokuwa akienda,
Alifika njiani,
Kaanguka kifudifudi,
Na sauti ikatoka.

Ni mimi! Ni Bwana!
Ambaye unatesa,
Haleluya simama,
Uende mjini,
Upate kuokoka.

## 73. UTUSIKIE SISI WANADAMU

Utusikie sisi wanadamu,
Dhambi zetu ni nyingi sana,
Tukisema hatuna dhambi za dunia,
Hapo twajidanganya wenyewe.

Unisamehe Mungu,
Mimi ninakulilia,
Majaribu ni mengi,
Unirudishe kwako Mungu nakuomba.

Tukikumbuka wakati wa yule Nuhu,
Wale wanyama waliokufa,
Kwa tabia ya dhambi za wanadamu,
Dhambi zetu kweli ni mbaya.

Tujitayarishe ndani ya roho zetu,
Kwamba kumfwata Mungu,
Tujiepushe na dhambi za wanadamu,
Tutapata raha ya milele.

## 74. UPENDO

Nikisema na lugha zangu,
Kushinda malaika,
Lakini sina upendo,
Mimi ni kitu bure.

Upendo huvumilia,
Upendo hauna choyo,
Upendo hauna chuki,
Upendo hauchoki.

Nikijuwa maarifa yote,
Na kujuwa siri zote,
Lakini sina upendo,
Mimi ni kitu bure.

Nikiwa na unabii,
Na imani timilifu,
Lakini sina upendo,
Mimi ni kitu bure.

Nikitoa mali zangu,
Niwape masikini,
Lakini sina upendo,
Mimi ni kitu bure.

Nikitoa mwili wangu,
Uungue motoni,
Lakini sina upendo,
Mimi ni kitu bure.

## 75. NIKIFIKIRI DUNIA HII

Edit with WPS Office

Nikifikiri dunia hii,
Mwisho wa yote umesongea,
Ugomvi mwingi na machafuko,
Kati ya mandugu na majirani.

Vitina vingi upendo hakuna,
Neno la Mungu si kitu kwao,
Yametimia maandiko ya Bwana,
Mwisho wa yote umesongea.

Na tukumbuke siku za Nuhu,
Pia wakati wa Sodoma na Gomora,
Watufikia tukae macho,
Neno la Mungu latuambia.

Tazama sana na uchunguze,
Watu waovu wote waongo,
Wapenda sifa za dunia hii,
Wamesahau neno la Mungu.

## 76. KATIKA BUSTANI MWA EDENI

Katika bustani mwa Edeni,
Mulikuwa na watu wawili,
Wa kwanza jina lake ni Adamu,
Wa pili mkewe Eva.

Kaini, ulikiwa u mwana wa Adamu,
Kaini, mbona ulimuuwa ndugu yako,
Eeh Kaini, damu ya ndugu yako yanitesa,
Kaini nitakulaani.

Hivi leo wako Kaini wengi,
Wadanganyifu mbele za Mungu,
Kwa kutoa matoleo yao,
Hizi peni mbili.

Mungu alimuuliza Kaini,
Yuko wapi ndugu yako,
Kaini akamjibu sijui,
Wala sitambui.

## 77. BWANA MUNGU

Bwana Mungu nashangaa kabisa,
Nikitazama kama ulivyo,
Nyota ngurumo vitu vingi vyote
Viumbwavyo kwa uwezo wako.

Roho yangu na ikuimbie,
Jinsi wewe ulivyo mkuu,
Roho yangu na ikuimbie,
Jinsi wewe ulivyo mkuu.

Nikitembea pote duniani,
Ndege huimba nawasikia,
Milima hupendeza macho sana,
Upepo nao nafurahia.

Nikikumbuka kama wewe Mungu,
Ulivyompeleka mwanao,
Afe azichukue dhambi zetu,
Kuyatambua ni vigumu mno.

Yesu mwokozi atakaporudi,
Kuwa nasi hapa duniani,
Nitamshukuru na kuimba milele,
Wote wajue jinsi alivyo.

## 78. BWANA NI MCHUNGAJI

Bwana ni mchungaji wangu,
Sitapungukiwa na kitu,
Hunilaza penye majani mabichi,
Huniongoza kwa maji matulivu.

Hakika wema nazo Fadhili zitanifuata mimi,
Nitakaa nyumbani mwa Bwana,
Siku zote za maisha yangu.

Hunihuisha nafsi yangu,
Huniongoza kwa njia za haki,
Nipitapo bondeni mwa mauti,
Sitaogopa wewe u nami.

Gongo lako na fimbo yako,
Vitanifariji mimi,
Waandaa meza mbele yangu,
Machoni pa watesi wangu.

## 79. TWASIKIA MWITO

Twasikia mwito kutoka mbali,
Tumeni injili,
Roho za watu na zionekane,
Tumeni injili.

Tumeni nuru ya injili,
Ing'are duniani.
Tumeni nuru ya injili,
Ing'are duniani.

Tumeitwa kueneza injili,
Tumeni injili,
Sadaka twaziweka msalabani,
Tumeni injili.

Natuombe neema ienee,
Tumeni injili,
Na roho wa Kristo aonekane,
Tumeni injili.

Tusichoke kazi ni kwa upendo,
Tumeni injili,
Taji ya uzima tupate mwisho,
Tumeni injili.

## 80. TAFUTENI KWANZA UFALME

Tafuteni kwanza ufalme wa Mungu,
Na haki yake,
Vitu hivi vyote mtaongezewa,
Halelu, Haleluya.

Haaleluya, Haleluya,
Halelu, haleluya.

Uombacho chochote utapewa,
Tafuta upate,
Bisha mlango utafunguliwa,
Halelu, Haleluya.

Ndimi njia, ukweli na uzima,
Yesu alisema,
Mtu haji kwa Baba ila kwangu
Halelu, Haleluya.

## 81. SAUTI YA MCHUNGAJI

Sauti ya mchunga wetu,
Twaisikia kwa mwitu,
Anaita kondoo zake,
Waliotoroka kwake.

Walete, walete,
Kutoka dhambini walete,
Walete, walete,
Nawalete kwake Yesu.

Nani amsaidiaye,
Yesu wokasa apate,
Nani atakayeleta,
Wale waliopotea.

Sauti zao nyikani,
Hata kutoka mlimani,
Tumesihiwa na Bwana,
Kuwaleta na salama.

## 82. WIVU NI MBAYA

Wivu ni mbaya mimi nakuonya,
Ulifanya Yusufu wa Yakobo,
Akauzwa huko Misiri,
Na ndugu zake kwa kumuonea.

"Ooh! Yusufu, mwana wangu,
Siamini macho yangu!" Yakobo alilia,
"Kwamba ni wewe uliyekufa,
Na kumbe uko Misiri!" Yakobo alilia.

Walipofika nyumbani kwa baba,
Walimudanganya kwamba Yusufu,
Ameliwa na mnyama mbaya,
Yakobo alihuzunika sana.

Edit with WPS Office

Yusufu alipokataa kuzini,
Mwanamke alimnyang'anya nguo,
Na kumshtaki kwa bwana wake,
Kwamba Yusufu ni mwenye dhihaka.

## 83. KUNA KIWANJA KIMOJA KITEULE

Kuna kiwanja kimoja kiteule,
Cha kusimama watu wote,
Kutoa kazi za kila mwanadamu,
Alizopewa na Mungu.

Wengine watafukuzwa, ondoka!
Sikujui sikujui mimi,
Kazi zako na talanta ulizopewa,
Ulizika chini wewe.

Watakuwa wakilia hoi! Hoi!
Tulifanya kazi za bure,
Watakimbia huku na huko pia,
Wakisaga meno yao.

Bwana Yesu alikuja kuokoa,
Wanadamu kutoka dhambini,
Atakuja kuchukua walio wake,
Walioshwa na damu.

Yakupasa mwanadamu ujiulize,
Bwana Yesu atakaporudi,
Utasimama kulia au kushoto,
Wake mwana wa Mungu.

Edit with WPS Office